

**UFAPANUZI KUHUSU RIPOTI ZA MWAKA ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI (CAG) ZILIZOWASILISHWA KWA MH. RAIS TAREHE 27 MACHI, 2018**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (Iliyorekebishwa mwaka 2005), mnamo Machi 27, 2018, Mdhiliti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Juma Assad, aliwasilisha ripoti zake za Ukaguzi wa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2017 kwa Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli.

Licha ya tukio hili kurushwa mubashara na Kituo cha Televisheni cha Taifa (TBC1), kwa mujibu wa Ibara tajwa hapo juu, bado ripoti za CAG za Ukaguzi wa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2017 zitabaki kuwa za siri kwa umma hadi zitakapowasilishwa Bungeni. Tukio hilo la uwasilishaji linatarajiwa kufanyika kabla ya Aprili 12, 2018 katika kikao cha kwanza cha Bunge kitakachofanyika baada ya ripoti za CAG kuwasilishwa kwa Mh. Rais.

Hivyo, matokeo ya ukaguzi yatawekwa wazi kwa Umma baada ya ripoti hizi kuwasilishwa bungeni rasmi.

Hivyo, umma unapaswa kusubiri hadi hapo ripoti hizi zitakapowasilishwa rasmi Bungeni. Baada ya kuwasilishwa Bungeni, ripoti hizo zitapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (www.nao.go.tz). Pia, nakala ngumu za vitabu zitapatikana kwenye Ofisi zetu zilizopo katika mikoja yote nchini.

Aidha, CAG anapenda kutoa ufafanuzi kuhusu kauli yake aliyoitoa kuhusiana na mwenendo wa ukuaji wa Deni la Taifa kama alivyonyukuliwa wakati akiwasilisha ripoti hizo kwa Mhe. Rais.

Taarifa sahihi kuhusu mwenendo wa Deni la Taifa kwa mujibu wa Taarifa ya Maandishi ya CAG ni kwamba, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2017 lilikuwa Shilingi trilioni 46.08. Kati ya deni hilo, deni la ndani ni Shilingi trilioni 13.34, sawa na asilimia 29; na Deni la Nje ni kiasi cha Shilingi trilioni 32.75 trilioni, sawa na asilimia 71. Kwa hiyo, deni la nje ni asilimia 31 ya Pato la Taifa (GDP). Vilevile, Ukaguzi umebaini kuwa, Deni la Taifa kwa sasa ni himilivu.

Mdhiliti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Prof. Mussa Juma Assad anaomba radhi kwa usumbufu wowote uliojitokeza kwa wananchi.

Imetolewa na,


Sakina Mfinanga

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi